

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS,  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO



Telephone: 0262968010  
Fax: 0262968010  
Website: www.kilolodc.go.tz  
Email: ded@kilolodc.go.tz/ded.kilolo@iringa.go.tz

S.L.P2324,  
KILOLO  
Tanzania.



Unapojibu tafadhali taja;

Kumb.Na.KDC/027/2024-25/OWNSOURCE/W/01

13/08/2024

**TANGAZO LA KAZI KWA MAFUNDI KATIKA NYANJA ZA UJENZI WA BARABARA**

1. Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya anakaribisha maombi kwa Wananchi wote, Mafundi/Wajenzi, vikundi mbalimbali, Taasisi za Umma au binafsi wenye nia na uwezo wa kutekeleza kazi tajwa hapo chini kwa ubora na viwango vinavyokubalika.

**KAZI YA KUFANYA (ZABUNI) NI KAMA IFUATAVYO;-**

NAMBA YA MRADI	KAZI ZA KUFANYA
LGA/027/2024/2025/OWNSOURCE/W/01	<ul style="list-style-type: none"><li>• UJENZI WA KALVATI; na</li><li>• KUSAMBAZA KIFUSI ENEO LA KUEGESHA MAGARI LUNDAMATWE</li></ul>

2. Utekelezaji wa miradi hii utafanyika kwa njia ya 'FORCE ACCOUNT', Aidha ofisi ya Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo Ilula inatarajia kuanza ujenzi wa miradi hiyo mara baada ya kupatikana Mafundi kwa kazi husika.

**MASHARTI YA WAOMBAJI**

Mwombaji anatakiwa atimize masharti yafuatayo:

1. Mwombaji awe na barua ya utambulisho kutoka kwa Mtendaji wa Kijiji;
2. Mwombaji awe na "Account" ya Bank;
3. Kama ni kikundi kiwe na Hati ya Usajili;
4. Mwombaji ataje bei (OFFER) na Muda wa kufanya kazi kwa zabuni anayoomba;

5. Mwombaji alipe ada ya maombi Tshs.10,000/= (elfu kumi tu), Ofisi ya Mamlaka ya Mji Mdogo Ilula na fedha hizo hazitarejeshwa;

**NB: Nakala ya stakabadhi ya malipo iambatanishwe kwenye barua ya maombi**

6. Maombi yafungwe kwenye bahasha vizuri, juu ya bahasha iandikwe aina ya zabuni inayombwa bila kuonyesha alama yoyote ya sehemu maombi yanakotoka;
7. Mwombaji asiwe anadaiwa na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W);
8. Kablasha la Zabuni linapatikana katika ofisi ya Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Ilula Kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa saa **2:30** asubuhi hadi saa **9:30** alasiri isipokuwa siku za sikukuu na mapumziko;
9. Kwa waombaji ambao shughuli zao zinapaswa kusajiliwa na mamlaka husika watapaswa kuonesha uthibitisho wa usajili wao/vibali vya kuruhusu kufanya kazi hizo;
10. Mwombaji awe na Mdhamini mmoja (1) mwenye makazi au mali zisizohamishika;
11. Waombaji ni lazima waoneshe anwani zao kamili na mahali ofisi zao zilipo;
12. Maombi hayo yatumwe kwa;

Katibu,  
Kamati ya Manunuzi,  
S.L.P 2324,  
**KILOLO**

13. Maombi yaletwe kwa mkono Ofisi ya Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo Ilula;
14. Maombi ambayo hayatazingatia masharti yaliyotajwa hapo juu hayatafikiriwa wala kushughulikiwa;
15. Kamati ya Manunuzi itajadili na kuteua Fundi atakae pendekezwa na kamati ya Tathimini na kupitishwa kuwa anafaa kwa kazi husika;
16. Maombi yatakayofika baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha zabuni hayatapokelewa; na
17. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **20/08/2024** saa **4.00** asubuhi na zabuni zitafunguliwa saa **4.30**; Asubuhi hiyo hiyo katika Ukumbi wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Ilula.

  
Hassan J. Mnyikah

Mkurugenzi Mtendaji (W)

**KILOLO**

**MKURUGENZI MTENDAJI WA WILAYA  
KILOLO**